# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS,
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# RISALA YA UTII KWA MHESHIMIWA DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KATIKA WILAYA YA RUANGWA
## TAREHE 23 MEI, 2017



***"SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA NCHI YETU''***

MKUU WA WILAYA
S.L.P. 1
**RUANGWA**

**MAGUFULI, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA KATIKA WILAYA YA RUANGWA TAREHE 23 MEI,2017.**

## 1.0 UTANGULIZI.

***Mheshimiwa Rais,*** Tunayo furaha kubwa kuupokea na kuukimbiza Mwenge wa Uhuru katika wilaya ya Ruangwa. Tunawakaribisha kwa moyo mkunjufu Wakimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa mwaka 2017 Ndugu Amour Hamad Amour **(KIONGOZI)** kutoka Kaskazini Unguja**,** Salome Obadia Mwakitalima kutoka Katavi**,** Shukran Islam Msuri kutoka Mjini Magharibi**,** Frederick Joseph Ndahani kutoka Singida, Vatima Yunus Hassan kutoka Kusini Pemba na Bahati Mwaniguta Lugodisha kutoka Geita.

Sisi wananchi wa wilaya ya Ruangwa tunafahamu vema umuhimu wa Mbio za Mwenge wa Uhuru. Baadhi ya mambo muhimu yaletwayo na Mwenge wa Uhuru ni pamoja na upendo, amani na mshikamano kwa watanzania wote bila kujali tofauti zao za kidini, rangi, kabila na itikadi za kisiasa.

***Mheshimiwa Rais,*** Wilaya ya Ruangwa ni moja kati ya wilaya tano za Mkoa wa Lindi. Ina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 2,560. Kiutawala ina jimbo moja la Uchaguzi, Tarafa 3, Kata 22, Vijiji 90 na Vitongoji 436. Kwa sasa wilaya inakadiriwa kuwa na watu 137,340 (wanaume 66,286 na wanawake 71,054). Ongezeko la watu kwa mwaka ni asilimia 0.9 na msongamano wa watu kwa kila kilomita ya mraba ni 53.

***Mheshimiwa Rais,*** Shughuli kuu za uchumi kwa wakazi wa wilaya ya Ruangwa ni kilimo ambacho huajiri asilimia 90 ya wakazi wote. Shughuli zingine za kiuchumi ni ufugaji, viwanda vidogo vidogo, ufugaji nyuki, Biashara ndogondogo, uchimbaji wa madini na ajira rasmi. Pato la mkazi wa Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa kwa mwaka linakadiriwa kuwa shilingi 1,679,000.

## 2.0 TATHMINI YA MIRADI ILIYOHUSIKA KATIKA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA MWAKA 2016.

***Mheshimiwa Rais,*** Katika mbio za mwenge wa uhuru kwa mwaka 2016 ulipitia miradi saba (7) yenye thamani ya shilingi 808,282,050.00 Miradi miwili (2) iliwekewa mawe ya msingi, mradi mmoja (1) ulizinduliwa, miradi minne (4) ilitembelewa. Miradi miwili iliyowekewa mawe ya msingi imekamilika. Miradi yote iliyohusika katika mbio za mwenge wa Uhuru mwaka 2016 inaendelea kutoa huduma kwa jamii.

## 3.0 TATHMINI YA MIRADI ILIYOHUSIKA KATIKA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA MWAKA 2017.

**Mheshimiwa Rais,** Mwaka 2017, miradi yenye thamani ya shilingi bilioni mbili milioni miatano ishilini na tano themanini na sita elfu miambili orobaini na tatu (**shilingi 2,525,086,243.00)** imezinduliwa, kutembelewa na kuwekewa mawe ya msingi na mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mchanganuo ufuatao:-

- Serikali Kuu imechangia shilingi 1,498,788,266.00 sawa na asilimia 59.35
- Halmashauri ya Wilaya imechangia shilingi 187,874,094.00 sawa na asilimia 7.44
- Wananchi wamechangia shilingi 80,101,077.00 sawa na asilimia 3.17
- Wafadhili wamechangia shilingi 758,322,806.00 sawa na asilimia 30.04

Miradi iliyotembelewa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 imehusisha sekta za Afya, Elimu, Maji, Barabara, Kilimo (usindikaji mazao), Mifugo na Maendeleo ya Jamii (Ujasiriamali na Vijana).

## 4.0 MICHANGO YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2017.

***Mheshimiwa Rais,*** Katika kufanikisha shughuli za mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017, Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa kushirikiana na wananchi, Taasisi na wadau mbalimbali wa maendeleo wamechanga jumla ya shilingi 23,668,000.00 na vitu vingine vyenye thamani ya shilingi 1,537,500.00. Mchango huu ni sawa na asilimia 91 ya lengo la kuchanga shilingi 27,796,400.00. Kati ya fedha hizo shilingi 19,960,235.00 sawa na asilimia 79 zimetumika kwa ajili ya kufanikisha maandalizi ya mapokezi ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 na shilingi 5,245,265.00 sawa na asilimia 21 ya fedha zilizochangwa zimetumika kuchangia miradi ya maendeleo inayotekelezwa na wananchi ambayo imehusika katika mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017.

## 5.0 UJUMBE WA MWENGE WA UHURU MWAKA 2017.

***Mheshimiwa Rais,*** Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 ni **"Shiriki kukuza uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu''.** Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa inaendelea kuimarisha viwanda vidogovidogo vilivyopo 51 kwa kuwapatia mafunzo usimamizi wa miradi, mikopo na tenda ili waweze kujipatia mapato na kujiendesha.

Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017 Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa katika kutekeleza dhana ya kukuza uchumi wa viwanda imetenga eneo lenye ukubwa wa jumla ya ekari 100 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo vidogo na vya kati. Kati ya eneo hilo ekari 10 zimetolewa kwa mwekezaji (Mount Meru Group of Companies) kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti. Ujenzi wa kiwanda hiki unatarajiwa kuanza Julai, 2017.

Kikundi cha Wabanguaji wa Korosho Ruangwa (WAKORU) kimetengewa eneo la ekari 4.2 na kupatiwa fedha shilingi 14,520,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho. Kiwanda hiki kipo katika hatua za ukamilishwaji na kinatarajia kuanza kazi katika msimu wa mavuno ya korosho wa mwaka 2017/2018.

Aidha Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa imetenga shilingi 221,365,338.00 katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya kuwezesha vikundi vya vijana na wanawake ili waweze kutekeleza shughuli za uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo hususan vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Aprili, 2017 Halmashauri imetoa shilingi 110,000,000.00 kwa ajili ya kukopesha vikundi 43 ambapo 12 ni vya vijana na 31 ni vya Wanawake. Pia SACCOS 2 za vijana na wanawake zimekopeshwa. Kati ya vikundi vilivyokopeshwa, vikundi 3 vinajishughulisha na viwanda vidogo vya kukamua mafuta ya alizeti, utengenezaji wa batiki na utengenezaji wa sabuni za maji.

## 6.0 JUHUDI ZA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI.

***Mheshimiwa Rais,*** Katika jitihada za kudhibiti maambukizi ya virusi vya UKIMWI, Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 umebeba kauli mbiu ya "***Tanzania bila maambukizi mapya***, ***Unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI inawezekana ifikapo 2030".***

Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa imeweka mapambano dhidi ya UKIMWI kuwa ni agenda ya kudumu na inaendelea kutoa elimu ya UKIMWI katika makundi ya vijana, walemavu, wazee, watumishi, viongozi wa dini, wakunga wa jadi, mangariba na waganga wa jadi. Uhamasishaji wa upimaji wa afya kwa hiari unaendelea ambapo kuanzia Julai, 2016 hadi Aprili, 2017, jumla ya watu 25,995 wamepimwa kwa hiari na wengine kwa kushawishiwa, wakiwemo wanaume 9,556 na wanawake 16,439. Kati ya idadi hii watu 651 waligundulika kuwa na Virusi vya UKIMWI wakiwemo wanaume 208 na wanawake 443.

Kiwango cha maambukizi mapya ya UKIMWI katika Wilaya yetu kwa kipindi hiki ni 2.6% ikilinganishwa na 2.9% mwaka 2015 jambo linaloonesha mafanikio katika mapambano haya. Jumla ya vituo 37 vinatoa huduma ya upimaji wa Virusi vya UKIMWI. Aidha huduma endelevu ya dawa za kufubaza makali ya Virusi vya UKIMWI yaani ARVs zinapatikana katika vituo 13 vilivyosajiliwa hapa Wilayani. Elimu dhidi ya kujikinga na maambukizi ya VVU inaendelea kutolewa kwa jamii.

## 7.0 MAPAMBANO DHIDI YA MALARIA.

***Mheshimiwa Rais,*** Ugonjwa wa malaria unaendelea kuwa tatizo licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na taifa, wilaya na wadau mbalimbali. Mwenge wa Uhuru mwaka 2017 umebeba kauli mbiu ya **"Shiriki kutokomeza Malaria kabisa kwa manufaa ya jamii"** Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Aprili, 2017 Jumla ya wananchi 86,631 walipima ambapo kati yao wanaume walikuwa 40,516 na wanawake walikuwa 46,115 na kati ya hao 44,293 sawa na asilimia 51.13 waliripotiwa kuwa na maambukizi ya malaria ambapo wanaume ni 20,596 na wanawake ni 23,697.

Asilimia ya maambukizi imepungua kutoka 35% Juni 2016 hadi 26%, Machi, 2017. Maambukizi haya yamepungua kutokana na jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Halmashauri ikiwemo utoaji wa elimu ya kuzuia maambukizi ya malaria, kinga kwa wajawazito pamoja na matibabu sambamba na matumizi sahihi ya vyandarua.
Jumla ya vyandarua 21,202 vimegawiwa kwa Wanafunzi wa shule za msingi (16,482) na wajawazito na watoto wa chanjo ya surua ya kwanza (4,720). Halmashauri inaendelea kuwahamasisha wananchi kwenda katika vituo vya kutolea huduma za Afya kupima mara wanapohisi dalili za malaria. Pia vituo vyote vya kutolea huduma za afya vinapata dawa za kutosha za kutibu malaria. Jamii imehamasishwa kutunza mazingira na kufanya usafi ili kupunguza mazalia ya mbu.

## 8.0 JUHUDI ZA MAPAMBANO DHIDI YA MADAWA YA KULEVYA.

**Mheshimiwa Rais,** Kwa upande wa Dawa za Kulevya; Wilaya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inapambana na wale wote wanaojihusisha na uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya. Kuanzia Julai 2016 hadi April 2017 watu 58 wamekamatwa kwa kosa la kukutwa na pombe haramu ya moshi (gongo) ikilinganishwa na watu 20 mwaka 2015/2016. Jumla ya lita 1079 zilikamatwa ikilinganishwa na lita 185 kwa mwaka 2015/2016 na mitambo 10 ya utengenezaji wa pombe hiyo ilikamatwa.

Aidha, kwa kipindi hiki watu 20 wamekamatwa ikilinganishwa na watu 3 waliokamatwa 2015/2016 kwa kujihusisha na uuzaji na utumiaji wa bangi ambapo kilo 114 zimekamatwa ikilinganishwa na kilo 1.5 kwa mwaka 2015/2016.
Mafanikio haya yamewezekana kutokana na doria na misako katika maeneo mbalimbali ya Wilaya. Pia elimu kwa umma imeendelea kutolewa kwa kutumia vyombo vya habari hasa Redio Ruangwa FM, mikutano ya hadhara na makongamano mbalimbali ili kuongeza uelewa wa athari za madawa ya kulevya.

## 9.0 JUHUDI ZA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA:

**Mheshimiwa Rais,** Katika kutekeleza ujumbe wa kudumu wa mapambano dhidi ya rushwa chini ya kauli mbiu ; " ***Tuungane kwa pamoja dhidi ya rushwa kwa maendeleo,amani na usalama wa Taifa letu*****"**. Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa kwa kushirikiana na TAKUKURU imekuwa ikitoa elimu dhidi ya rushwa kwa kutumia njia mbalimbali kama vile semina, mikutano ya hadhara, makongamano na vipindi vya radio kupitia Redio Ruangwa FM kwa lengo la kuwapatia wananchi uelewa wa rushwa na kujua haki zao.
Aidha, klabu za wapinga rushwa zimeanzishwa katika shule zote 15 za sekondari kwa lengo la kuwajengea wanafunzi uelewa dhidi ya rushwa mapema ili watakapomaliza masomo na kuajiriwa katika sekta mbalimbali waweze kufanya kazi kwa uadilifu.

Pia Halmshauri ya wilaya ya Ruangwa kwa kushirikisha TAKUKURU kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017 imefanikiwa kuokoa fedha za umma kiasi cha shilingi 26,789, 600 ambazo zilikuwa zimepotea kwa njia za rushwa na kuzirudisha serikalini.

## 10. HITIMISHO.

***Mheshimiwa Rais,***Tunakupongeza wewe binafsi na serikali yetu kwa kuendeleza kwa vitendo misingi ya taifa letu ya umoja, amani na utulivu unaotuwezesha kufanya shughuli za maendeleo kwa ufanisi. Tunakuombea Mungu akupe maisha marefu na afya njema.

Sisi wananchi wa Wilaya ya Ruangwa tunakuahidi kuwa tutatekeleza kwa vitendo ujumbe wa Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2017 ili kupata mafanikio zaidi ya kiuchumi na kijamii yatakayotuwezesha kuondoa umaskini katika Halmashauri yetu.

Aidha, tunawapongeza wakimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa mwaka 2017 kwa umahiri na ushupavu waliouonyesha katika Wilaya yetu ya Ruangwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema ili waweze kutekeleza kazi hii muhimu waliokabidhiwa na Taifa kwa ufanisi na usalama.

**MUNGU IBARIKI RUANGWA,**
**MUNGU IBARIKI TANZANIA.**
**NI SISI WANANCHI WA WILAYA YA RUANGWA**

Rukia Muwango
Kaimu Mkuu wa Wilaya
**Ruangwa.**